# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI
# MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

**660** **MALEZI YA ELIMU YA AWALI**

**Muda: Saa 3** **Ijumaa, 8 Mei 2009 Mchana**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A maswali **mawili (2)** kutoka B na swali **moja (1)** kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 36, sehemu B ina alam 40 na sehemu C ina alama 24.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

## SEHEMU A (Alama 36)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja dalili nne (4) zinazoonesha kuwa mwanafunzi wa Elimu ya Awali anajifunza.

2. Kwa kutumia mifano onesha aina kuu mbili (2) za uchunguzi wa mtoto wa Elimu ya Awali.

3. Katika Tanzania Elimu ya Awali imegawanyika katika sehemu kuu mbili:

   (a) Taja sehemu hizo

   (b) Eleza kwa kifupi tofauti zake

4. Taja nadharia kuu nne (4) zinazohusu kujifunza kwa mtoto.

5. Fafanua jinsi utakavyotumia njia ya maelekezo katika kumfundisha mtoto wa Elimu ya Awali.

6. Ainisha mambo manne (4) yanayoathiri ukuaji wa mtoto wa Elimu ya Awali.

7. Ni vitu gani vinavyomfanya mtoto wa Elimu ya Awali apende kujifunza?

8. Taja mwaka na wakati ambao Elimu ya Awali ilianzishwa hapa nchini Tanzania.

9. Unaelewa nini kuhusu ukuaji wa mtoto kimaono?

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii

10. Ukuaji wa mtoto unategemea nyanja mbalimbali. Jadili nyanja hizo kwa ufasaha.

11. Kwa nini umri wa kutoka kuzaliwa hadi miaka sita (6) ni muhimu kwa makuzi ya mtoto?

12. Kuna umuhimu gani wa kumshirikisha mtoto katika mchakato mzima wa ujifunzaji?

13. Eleza mambo ya kufanya unapochagua chumba cha Elimu ya Awali ili kiweze kumsaidia mtoto kujifunza.

## SEHEMU C (Alama 24)

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

14. Bainisha watoto wenye mahitaji maalumu na eleza jinsi utakavyowasaidia katika mazingira ya kujifunza.

15. Jadili matatizo yanayoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Awali.

16. Eleza mbinu utakazotumia ili kushirikisha watoto wengi unapofundisha darasa la Elimu ya Awali.

- Michezo
- nyimbo
- hadithi
- maonyesho
- maelezo
- Ziara tembezi
- maigizo
- Vitendo
- kuria

Lord help me.